JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA MANISPAA YA MUSOMA

Kumb. Na. HMM/P.40/VOL.XIII/11 Tarehe: 21 Novemba, 2024

KURUDIA TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Musoma amepokea kibali cha ajira kutoka kwa Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora chenye Kumb **Na. FA.97/288/01/09** cha tarehe **25 Juni, 2024.** Hivyo anapenda kuwatangazia watanzania wote wenye sifa kutuma maombi kwa nafasi tatu (3) kama zilivyoainishwa kwa kuzingatia sifa tajwa:-

1.0 DEREVA DARAJA LA II NAFASI 03

1.1 MAJUKUMU YA KAZI

i. Kukagua gari kabla na baada ya safari ili kubaini hali ya usalama wa gari.
ii. Kupeleka watumishi maeneo mbalimbali kwenye safari za kikazi.
iii. Kufanya marekebisho madogo madogo ya gari.
iv. Kukusanya na kusambaza nyaraka mbalimbali
v. Kujaza na kutunza taarifa za safari zote katika daftari la safari
vi. Kufanya usafi wa gari na
vii. Kufanya kazi nyingine kadri atakavyoelekezwa na Msimamizi wake.

1.1.1 SIFA ZA MWOMABAJI

Awe na elimu ya kidato cha nne na Leseni daraja E au C ya uendeshaji magari ambayo amefanyia kazi kwa muda usioupungua mwaka mmoja bila kusababisha ajali. Awe amehudhuria mafunzo ya uendeshaji magari (Basic driving Course) yanayotolewa na

Chuo cha mafunzo ya ufundi stadi (VETA) au chuo kingine kinachotambuliwa na Serikali.

1.1.2 NGAZI YA MSHAHARA

Mshahara utalipwa kwa kuzingatia viwango vya Serikali **TGS B**

1.2 MHUDUMU WA JIKONI DARAJA LA II NAFASI (02)

1.2.1 KAZI NA MAJUKUMU

i. Kusafisha vyombo vya kupikia

ii. Kusafisha vyombo vya kulia chakula

iii. Kusafisha sehemu ya kulia chakula

iv. Kuwatayarishia Wapishi/Waandazi vifaa vya kazi

v. Kusafisha maeneo ya kupikia

1.2.2 SIFA ZA MWOMBAJI

Kuajiriwa wahitimu wa kidato cha IV wenye cheti cha mafunzo ya uhudumu wa jikoni cha mwaka mmoja (1) kutoka VETA au chuo kinachotambuliwa na Serikali.

1.2.3 MSHAHARA

Mshahara utalipwa kwa kuzingatia viwango vya Serikali **TGOS A**

1.3 MSAIDIZI WA MAENDELEO YA JAMII DARAJA LA II– NAFASI 01

1.3.1 KAZI YA MAJUKUMU

i. Kuratibu shughuli za maendeleo katika Mtaa zikiwemo za wanawake na watoto na zikizingatia jinsia.

ii. Kuwezesha jamii kushiriki katika kubuni kupanga, kutekeleza, kusimamia, kutathimini mipango/ miradi ya maendeleo.

iii. Kuhamasisha na kuwawezesha wananchi kupanga, kutekeleza kazi za maendeleo ambazo ni pamoja na usafi wa mazingira, ujenzi wa shule, zahanati, majosho na ujenzi wa nyumba bora.

iv. Kuratibu shughuli za kupambana na UKIMWI

v. Kuratibu shughuli za Mashirika na Asasi zisizo za Kiserikali na za kijamii.

vi. Kusaidia shughuli za kinga za magonjwa ya watoto wadogo eneo la kituo

vii. Kuwa kiongozi wa kituo cha kulea watoto

1.3.2 SIFA ZA MWOMBAJI

Kuajiriwa wahitimu wa kidato cha IV waliofuzu mafunzo ya cheti kwenye fani ya Maendeleo ya Jamii katika vyuo vya Maendeleo ya Jamii au vyuo vingine vinavyotambuliwa na Serikali.

1.3.3 MSHAHARA

Mshahara utalipwa kwa kuzingatia viwango vya Serikali **TGS B**

MASHARTI YA JUMLA

i. Waombaji wote wawe Raia wa Tanzania wenye umri usiozidi miaka **45** na usiopungua umri wa miaka **18**

ii. Waombaji wote waambatanishe na cheti cha kuzaliwa

iii. Waombaji waambatanishe maelezo binafsi **"CV"** yenye anuani na namba za simu na majina ya wadhamini (Referees) wa kuaminika

iv. Waombaji wote waweke nakala za vyeti vya taaluma, na vyeti vya kidato cha Nne na sita kwa wale waliofikia kiwango hicho na vyeti vya kuhitimu mafunzo mbalimbali kwa kuzingatia sifa za kazi husika kwenye ajira portal.

v. Testimonials "Provisional result", "Statement of Result", hati za matokeo ya matokeo ya kidato cha Nne na Sita HAVITATAKUBALIWA

vi. Waombaji wote waweke picha mbili "passport Size", ya hivi karibuni katika ukurasa wa ajira portal

vii. Waombaji wote waliosoma nje ya Tanzania wahakikishe vyeti vyao vimehakikiwa na vimethibitishwa na mamlaka husika ya TCU, NACTE na NECTA).

viii. Waombaji waliostaafishwa katika Utumishi wa Umma hawaruhusiwi kuomba isipokuwa kama wana kibali kutoka kwa Katibu Mkuu Kiongozi.

ix. Waombaji kazi ambao tayari ni waajiriwa **katika nafasi za kuingilia walioko katika Utumishi wa Umma wasiombe na wanatakiwa kuzingatia maelekezo yaliyo katika Waraka Na. CAC.45/257/01/D/140 wa tarehe 30 Novemba, 2010**

x. **Uwasilishaji wa taarifa na sifa za kughushi wahusika watachukuliwa hatua za kisheria.**

xi. Mwisho wa kutuma maombi ni tarehe **30/11/2024.**

xii. MUHIMU Kumbuka kuambatisha barua yako ya maombi ya kazi iliyosainiwa pamoja na vyeti vya elimu, anuani ya barua hiyo ielekezwe kwa;-

MKURUGENZI WA MANISPAA,
HALMASHAURI YA MANISPAA YA MUSOMA,
S.L.P 194,
MUSOMA

xiii. Maombi yote yatumwe kwenye mfumo wa kielekroniki wa Ajira (Recruitment Portal) kupitia anwani ifuatayo: https://portal.ajira.go.tz/ (Anuani hii pia inapatikana kwenye tovuti ya Sekretarieti ya Ajira kwa kuingia sehemu iliyoandikwa 'Recruitment Portal').

xiv. Maombi yatakayowasilishwa nje ya utaratibu ulioainishwa katika tangazo hili **HAYATAFIKIRIWA.**

Imetolewa na

MKURUGENZI WA MANISPAA
HALMASHAURI YA MANISPAA
MUSOMA